# Swahili B – Higher level – Paper 1
# Swahili B – Niveau supérieur – Épreuve 1
# Swahili B – Nivel superior – Prueba 1

Friday 4 November 2016 (afternoon)
Vendredi 4 novembre 2016 (après-midi)
Viernes 4 de noviembre de 2016 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

8 pages/páginas

8816 – 2316
© International Baccalaureate Organization 2016

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

https://xtremepape.rs/

Blank page
Page vierge
Página en blanco

https://xtremepape.rs/

**Kifungu A**

# Kanga, vazi linalowakilisha utamaduni wa Kitanzania

❶ Ingawa Tanzania kuna makabila zaidi ya 120 yenye mavazi tofauti kanga ni miongoni mwa mavazi yanayowakilisha utamaduni wa Watanzania kwa kuwa linatumiwa takribani na makabila yote.



❷ Kanga ni kipande cha kitambaa kilichorembwa kwa maua, rangi mbalimbali na kuchapishwa maneno. Maneno haya hutoa tafsiri kulingana na utamaduni wa jamii husika. Doti moja ya kanga ni kipande cha kitambaa chenye upana usiozidi mita moja na urefu usiozidi mita nne ambacho hukatwa katikati na kupata vipande viwili vyenye kimo sawa.

❸ Vazi la kanga ni maarufu zaidi kwa Waswahili wa maeneo ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki hasa Tanzania katika pwani ya Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Kilwa, Bagamoyo na Kenya hasa Mombasa na Malindi. Kwa mujibu wa historia ya uvaaji wa kanga, vazi hilo lilianza kutumika na kupata umaarufu tangu karne ya 19 ambapo kanga zilivaliwa zaidi na wanawake katika sehemu zenye joto.

❹ Kuenea kwa vazi hilo katika ukanda wa pwani kuliwavutia pia watu wa bara ambao walianza kutumia kanga kama vazi la ziada na kuwafanya wageni wanaotembelea Afrika Mashariki kuvutiwa na jinsi kanga inavyotumiwa na watu wa makabila mbalimbali kwa matumizi mbalimbali. Uvaaji wa kanga hutoa tafsiri tofauti kulingana na haja ya wavaaji wenyewe.

❺ Kuna wale wanaoona kuwa kanga ni vazi la ziada kwa mwanamke ambapo huvaa nguo kisha juu hujitanda kanga kama nguo ya ziada. Wengine husema kuwa ni vazi maalum la siku ya harusi kwa wanawake, yaani Bibi harusi. Tafsiri ya wengi husema kuwa kanga ni nguo au vazi la kwanza kwa mtoto mchanga siku anayokuja duniani. Hata hivyo matumizi ya kanga ni mengi na baadhi ya makabila wanatumia kanga kama vazi maalum hususani wakati wa sala kwa wanawake wa Kiislamu.

❻ Pia joto linapokithiri baadhi ya watu huvaa kanga kwa kuwa ni vazi jepesi kwa ajili ya kupunguza joto. Kanga pia hutumika kama taulo ya kufuta maji baada ya kuoga. Vilevile, kanga hutumika kama sare maalum ya harusi kwa koo mbili zinazoungana ambapo sare ya kanga hutumika kama ishara ya kujenga umoja, upendo na mshikamano.

Lucy Lyatuu, *HabariLeo* (2015)



https://xtremepape.rs/

**Kifungu B**

## Fursa ya elimu – Zanzibar

❶ Tangu yafanyike mapinduzi matukufu ya watu wa Zanzibar, kumekuwa na mabadiliko katika fursa za elimu. Mahali pa elimu ya wachache pamechukuliwa na elimu ya wengi. Kabla hatujayachunguza mabadiliko haya vipi yamewapatia fursa za kupata elimu watoto wa wafanyakazi na wakulima, yatupasa tutupie jicho utaratibu wa elimu uliotolewa miaka ya nyuma.

❷ Zanzibar ilipokuwa chini ya utawala wa wachache fursa nyingi za elimu zilitolewa kwa tabaka. Ama kwa tabaka la mabwanashamba au kwa tabaka tawala na kwa nadra zilitolewa kwa watoto wa wanyonge waliokuwa na vipawa maalum ambavyo watoto wa matabaka ya mwanzo na ya pili hawakuwa navyo. Watoto wa tabaka la chini walipata elimu ya muda mfupi. Elimu waliyopata haikuwawezesha kushika dhamana muhimu za serikali. Nafasi walizoweza kushika ni za chini ambazo malipo yake pia yalikuwa ni madogo. Hata hizo nafasi walizozishika, mathalan, kusomesha shule za msingi, kusaidia kuuguza wagonjwa hospitalini au ukarani wa daraja la chini, zilikuwa chache mno. Kwa hivyo, ililazimu vijana wengi wakomee darasa la 7 au 8.

❸ Kukosa nafasi za kuendelea na masomo au kuajiriwa serikalini kuliwafanya vijana warudi vijijini ambako mfumo mbaya wa elimu ya kikoloni ulikwisha kuwatenga na wakulima. Elimu ya miaka saba au minane waliyoipata haikuweza kuwafanya wawe wakulima, kwani haikuwatayarisha kwa maisha ya baadaye. Mengi kati ya yale waliyojifunza hayakuhusu mazingira yao. Kwa hivyo, wanafunzi walibaki bado wageni katika nchi yao. Watoto wa wachache, wa matabaka tawala pamoja na waliomiliki mashamba na idadi ndogo mno ya watoto wa wanyonge wenye kipawa cha kupigiwa mfano, ndio walioweza kuendelea na skuli za sekondari na hata Chuo cha Makerere, Uganda na mwishowe Ulaya.

❹ Sasa Zanzibar ina utaratibu mpya wa elimu, utaratibu huu umeanzishwa baada ya mapinduzi. Lengo la mpango mpya wa elimu ni kuwakomboa wananchi kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Utaratibu huu uliojengwa juu ya usawa – bila kujali rangi au dini ya mtu unatoa fursa za elimu kwa wote ili kuwaunganisha watu na hatimaye kujenga jamii ya kijamaa. Katika kutayarisha mpango wa kuzigawa fursa za elimu, serikali ya wafanyakazi na wakulima ilichukua hatua zifuatazo; kwanza iliondoa ada za shule, pili, skuli zote zilizokuwa zikiendeshwa na makabaila zilichukuliwa na serikali.

❺ Serikali mpya haikutosheka na mabadiliko hayo; ikaamua kutoa fursa zaidi. Kabla ya mapinduzi kulikuwa na skuli tatu hapa Zanzibar zilizotoa elimu ya sekondari. Huko Pemba ilikuwa moja tu. Leo kuna shule kadhaa zinazotoa elimu ya sekondari ya kidato cha 1 hadi 3 na kuna madarasa yasiyopungua 40 yanayotoa elimu ya kidato cha 4. Vyuo navyo vimeongezeka. Kwa mfano, kuna vyuo vinavyowatayarisha wanafunzi kwa kilimo, uvuvi na ufundi. Lakini, mabadiliko makubwa kabisa yanaonekana katika elimu ya msingi ambayo imekusudiwa kuwapatia nafasi watoto wote waliofikia umri wa kuingia shule.

Haji Ameir, *Mazoezi ya Ufahamu* (1981)

https://xtremepape.rs/

**Kifungu C**

# Mazingira machafu na athari zake

❶ Kuwa na afya bora, pamoja na kuendelea kuwa na afya bora ni wajibu wa kila binadamu. Tunahitaji kuwa na miili yenye afya bora na nguvu ili tuweze kuendelea na shughuli zetu za kila siku katika ujenzi wa taifa. Mtakubaliana na mimi kuwa ili taifa lipate maendeleo ya haraka, halina budi kuwa taifa la watu wenye afya njema. Ni wazi kabisa katika nyakati hizi, na katika jamii tunayoishi, na katika vijiji, miji na majiji, kiwango cha usafi wa mazingira ni duni sana na hamna viwango maalum vilivyowekwa katika kuyaweka mazingira safi.

❷ Nadhani kinachotufanya tuwe hivi na kutojali kuyaweka mazingira yetu yawe safi, ni mazoea tuliyokuwa nayo na tumekulia katika mazingira yasiyo safi hali iliyotufanya tuzoee mazingira yasiyo safi. Ona vyakula viuzwavyo mtaani bila kufunikwa katika vumbi jingi na moshi mzito utokanao na magari na shughuli nyingine, lakini tunanunua na kula. Ni kweli kuwa ulaji huo hupelekea kupata magonjwa ambayo hutufanya tujikute katika hospitali mbalimbali tukihangaika kuokoa maisha yetu. Ni gharama kwetu na gharama kwa taifa.

❸ Tazama wasafiri wa vyombo mbalimbali vya majini, mijini, katika mikoa na hata nje ya nchi watupavyo taka katika mazingira bila kujali uharibifu, bila kujali kama ni mbuga ya wanyama, kama ni chanzo cha maji na hata bila kujali kama ni msitu wa hifadhi.

❹ Kwa kuwa hatuna mazoea ya kutupa na kuharibu taka katika njia iliyo sahihi, siyo ajabu kuona taka za majumbani na hata viwandani zikiwa zimetupwa ovyo mitaani, barabarani, katika majengo ambayo hayatumiki, katika mitaro, mtoni, chini ya madaraja, fukwe za bahari na maziwa, mbuga za wanyama na hata katika misitu. Taka hizi hutoa harufu mbaya na kali hata kama mtu anapita mita kadhaa mbali na taka hizo. Pia ni kero kubwa kuishi katika baadhi ya makazi kutokana na rundo kubwa la taka katika maeneo hayo zitoazo harufu kali na sumu mbalimbali zinazowaathiri kiafya wakazi hao.



❺ Taka zinazozalishwa na familia zaweza kuwa hatari zisipotupwa na kuharibiwa katika njia iliyo sahihi. Taka hizi zaweza kupelekea milipuko ya magonjwa hatari, na zinapoachwa wazi zinaweza kuchafua mazingira, na kusambaza magonjwa kupitia upepo unaovuma, wadudu kama nzi na mende, na pia uambukizo wa magonjwa waweza kusambazwa kupitia njia ya upumuaji. Vimelea vya magonjwa vyaweza pia kuingia katika vinywaji visivyofunikwa, vyakula vilivyoachwa wazi barabarani na kusababisha magonjwa kama kuhara damu, kipindupindu, homa ya tumbo, minyoo, kichefuchefu na kutapika.

❻ Kwa hiyo basi, kuyaweka mazingira yetu katika hali ya usafi, kutatuepusha na matatizo mengi yakiwemo magonjwa mbali mbali. Pia tutapunguza gharama kubwa zitumikazo katika matibabu ya magonjwa hayo. Nchi yenye watu wenye afya ni nchi yenye mazingira mazuri na safi kwa ukuaji wa uchumi wake.

https://sayansiyaafya.blogspot.co.uk (2015)



https://xtremepape.rs/

**Kifungu D**

# Teknolojia na mtindo wa maisha



❶ Hamjambo wapenzi wasikilizaji na karibuni kujiunga nami katika makala hii ambayo huangazia taathira za teknolojia mpya za mawasiliano na habari na hasa intaneti katika mtindo wa maisha ya mwanadamu. Katika miaka ya awali ya utumizi wake, intaneti ilikuwa ikitumika na watu wachache tu lakini sasa watu wote wa dunia wanaweza kutumia intaneti. Mtandao huu uliojaa maelezo na ambao pia una uwezo wa mawasiliano ambao hutumiwa na watu wa matabaka yote sasa umekuwa kitu cha kawaida katika dunia ya leo. Kustawi kwa kasi kwa utumizi wa intaneti ni nukta ambayo haiwezi kupingika. Kwa upande mwingine, mabadiliko katika vifaa vya mawasiliano ya kisasa ni jambo ambalo limepelekea kutikisika misingi ya suhula za zamani za mawasiliano. Wataalamu na wanafikra wanaweza kuchangia pakubwa katika teknolojia za kisasa kwa kuvumbua mambo ambayo yanaweza kuwa na faida kwa jamii. Hivi sasa kufuatia ustawi wa kasi wa intaneti tunashuhudia kuongezeka kwa idadi ya watumizi wake kiasi kwamba masuala mengi zaidi ya mtindo wa maisha yanaathiriwa na teknolojia hii.

❷ Dhana ya "mtindo wa maisha" ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika karne ya 20 na Alfred Adler mwanasaikolojia au mtaalamu wa elimu ya nafsi kutoka Ujerumani. Hata hivyo, mtazamo wake kuhusu "mtindo wa maisha" ulikuwa wenye muelekeo wa kisaikolojia tu na hivyo haukuangazia mielekeo mingine kama vile ya kijamii. Hivi sasa nadharia ya "mtindo wa maisha" ina uhusiano wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja na taaluma za saikolojia, tabia, uchumi, usimamizi, mauzo, soshiolojia, utamaduni na sayansi ya mawasiliano. Moja ya sifa maalumu za "mtindo wa maisha" ni kuwepo uwezo wa kuchagua na kuwa chaguo hili hugeuka na kuwa simulizi ya mtu binafsi ambayo huweza kumuarifisha miongoni mwa wengine. Kuna mielekeo miwili katika kuarifisha au kubainisha maana ya "mtindo wa maisha". Muelekeo wa kwanza ni kuhusu tabia au mwenendo na pili ni thamani za kimaisha. Pamoja na hayo, kumekuwepo na changamoto nyingi katika kuchunguza kadhia ya "mtindo wa maisha" na hivyo bado kunahitajika utafiti zaidi na wa kina. Pamoja na hayo, kuibuka kwa teknolojia mpya katika maisha ya mwanadamu kumepelekea kujitokeza swali kuhusu "uwezo wa kuchagua" kama moja ya sifa za "mtindo wa maisha".

https://xtremepape.rs/

❸ Siku za nyuma, eneo la kuishi, kufanya kazi na kadhalika lilikuwa na nafasi ya kimsingi katika kuunda utambulisho wa kijamii wa mwanadamu. Hii ni kwa sababu mwanadamu alikuwa akiishi katika eneo dogo na hivyo utambulisho wake wa kijamii ulibainika kupitia uhusiano na maingiliano yake na watu aliokuwa akiishi karibu nao. Ni watu wachache tu waliokuwa na uhusiano na dunia ya nje ya miji au vijiji vyao na kwa msingi huo mila na desturi za kikaumu au kikabila zilikuwa na nafasi muhimu katika utambulisho wa watu. Kufuatia kuibuka kwa teknolojia mpya ya habari na mawasiliano, nafasi ya eneo si muhimu sana katika kuunda utambulisho wa mtu binafsi.

http://kiswahili.irib.ir (2015)



https://xtremepape.rs/

**Kifungu E**

# Tumbombele mla misitu

❶ Miti ilifurahia amani isiyo na kipimo hadi siku ambayo Tumbombele aliteuliwa kuwa waziri wa misitu katika nchi ya Mbalungi. Tumbombele alikuwa amechaguliwa na wakazi wa eneo bunge la Bumbi katika uchaguzi wa mwaka uliotangulia. Kabla ya hapo, miti ilishangilia hewa mwanana iliyovuma vuu vuu! Kutoka mti mmoja kuelekea mwingine. Kuteuliwa kwa Tumbombele hakukupokelewa kwa furaha na miti. Badala yake kulizua kilio na huzuni.

❷ Tumbombele alikuwa mbumbumbu mwenye elimu duni. Ungemuuliza majina ya miti ya kiasili hangeweza kukutajia hata mmoja. Historia yake ya elimu iligubikwa kwenye giza totoro. Ilisemekana mara alifika hadi kidato cha kwanza. Wakati mwingine ilisemekana kuwa hajawahi kuona mlango wa shule ya upili. Masomo yake yaligubikwa na utata.

❸ Kimbunga kikali cha kisiasa kilichovuma nchini humo mwaka uliotangulia kilipeperusha hata wasiokuwa na ajenda yoyote hadi wakaingia bungeni. Hatimaye waliteuliwa kuwa mawaziri mradi tu wawe wakereketwa wa chama tawala licha ya elimu yao pungufu. Mmoja wa wale waliofaidika kutokana na vuguvugu hilo alikuwa Tumbombele.

❹ Mara tu baada ya kuteuliwa waziri wa misitu, Tumbombele alifanya ziara ya kujifahamisha hali ya misitu ilivyokuwa nchini humo. Kwanza alitembelea msitu wa Mvule. Maafisa wa misitu, walinzi wa misitu, machifu na manaibu wao na wananchi walikuja kumsikiliza waziri mpya wa misitu. Hii pia ilikuwa sherehe ya kumkaribisha nyumbani baada ya kuteuliwa kuwa waziri.

❺ Tumbombele alisimama mbele ya uwanja akaanza kuhutubu:
"Serikali yetu inatambua umuhimu wa misitu. Inatambua miti ni uhai. Miti hutupatia hewa safi inayovuma kutoka kusini kuelekea kaskazini. misitu ni uhai. Asiyehifadhi miti hana nafasi katika Bumbi na nchini kwa jumla." Wananchi walimpigia makofi na ukemi kumshangilia. "Kuanzia sasa ni marufuku kukata miti hasa ya kiasili kwa shughuli zozote zile. Anayetaka kuozea jela ajaribu kukata miti ya kiasili ovyoovyo". Watu walimshangilia zaidi. Aliendelea kuzungumzia manufaa ya kuhifadhi mazingira na hasara ya kutofanya hivyo. Kisha mkutano ukafika mwisho wake. Watu walifumukana kuelekea makwao. Hotuba ya waziri Tumbombele ilijaa matumaini. Iliwapa watu wa Bumbi na nchi nzima ya Mbalungi uhai na mwamko mpya.

❻ Baada ya **[ – X – ]** yake ya kujifahamisha na hali ya misitu, Tumbombele alirudi jijini. Aliwaza na kuwazua kuhusu utajiri wa nchi ya Mbalungi. Alijisemea kimoyomoyo, "Mimi ni waziri wa misitu. Mtu huvuna apandacho. Si walisema kuwa mtu hujipatia **[ – 54 – ]** kutokana na kazi aifanyayo? Kwa nini nisijifaidi kutokana na **[ – 55 – ]** ninayosimamia? Nitafanya mipango". Kutoka siku, hiyo **[ – 56 – ]** cha kupata pesa kwa njia za mkato kilimwingia hadi mishipani.

Kobia John, *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007)

https://xtremepape.rs/